

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
14 Juni 2008**

Mahudhurio

Allan Edgar
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Husein Hamza Hamisi
Juma Hassan Chibaya
Kibwana Mohammad Msiga
Markus Weise
Paulo Atibu Hatibu
Sudi Saidi Ramadhan

Ofisi

Mejah bado hajapaka rangi ya nembo na jina la UWABA kwenye ofisi mpya na atakuwa na safari wiki hii pia.

Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund

Wakati wa wiki Andrew wa Ben Bikes alitutumia manual wanayotumia kufundisha usalama wa baisikeli Afrika Kusini na tulisoma kwenye mkutano. Mawazo kuibadilisha ifai kwa mazingira ya Tanzania yalikuwa: sehemu ya wapi kuendesha baisikeli kuonyesha aina za barabara za Dar es Salaam, iwe na mafundisho kuhusu husheshima watembea kwa miguu, na kuonyesha baisikeli ambazo ni kawaida Dar es Salaam. Elaine alisema ataanza kutafsiri na msaada wa wanachama wengine.

Tulikubali kuwapa Chuo cha Usafirishaji nakala ili watoe mawazo yao.

Markus na Juma walitembelea HUWATA Ijumaa baadala ya jumanne kwa sababu HUWATA walikuwa na mkutano na wizara ya miundombinu. Bado hawajaandika repoti ya shule walizotembelea. Watatembelea Kigamboni na Markus na Juma jumatatu.

TANROADS na barabara mpya

Markus na Juma walitembelea TANROADS ijumaa na aliongea na mkuu wa usalama barabarani. Hajaweza kujibu maswali vizuri lakini alisema atafuatalia. Tutaandika barua nyingine kuomba taafira na Markus ataenda tena wiki ijayo.

Kodi

Elaine aliandika barua kuomba taarifa kuhusu kodi. Ataibadilisha kuomba taarifa kuhusu kodi za Afrika Mashirika pia.

Mambo ya hela

Wakati wa wiki Ally Saidi Mwishehe alimpa Juma Tsh 7,000 kama kodi ya guta.